

PAROKIA YA MT. GASPAR DEL BUFALO

MBEZI BEACH, P. O. BOX 167,
JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM, TANZANIA. Phone No.0222618108/0754518548I
Email: *gasparparish@yahoo.com*

1: HISTORIA YA PAROKIA YA MT. GASPAR DEL BUFALO NA KITUO CHA HIJA (SHRINE).

PAROKIA na Kituo cha Hija cha Mt. Gaspar Del Bufalo
(Shrine) kilianza Kama Kigango cha Mwenyeheri Maria De Matias Mwaka 1990 katika eneo hili la Mbezi Beach ikijulikana kama MBEZI **MACHAKANI.**Viongozi wa Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi kutoka Italia
(Mapadre Don Evaldo na Don Valenzano Wahasibu Wastaafu) Walikuwa wakitembelea Tanzania Mara kwa Mara wakati wa Uongozi wao, Walipata wazo la kwamba watakapoadhimisha **JUBILEI YAO YA DHAHABU** wanataka Kujenga hapa Tanzania (**SHRINE)** kwa Heshima ya MT. **GASPAR DEL BUFALO.** Viongozi wa Shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ya Yesu Tanzania wakati huo chini ya **Padre Vincent Bosel** walipendekeza **SHRINE** hiyo ijengwe **DAR ES SALAAM katika Kigango cha Mwenyeheri Maria De Matias na hivyo Jina la Kigango likabadilishwa na kuitwa Mt. Gaspar Del Bufalo**.

Padre Dominico Altieri alikwenda kuonana na Askofu Mkuu wa Jimbo Kuu la
Dar es Salaam, Mwadhama Polcarp Kardinali Pengo (Askofu Mkuu Mstaafu sasa) ili kumuomba kujenga Shrine katika Jimbo Lake, Baba Kardinali alimkubalia ombi lake na kumuomba ajenge Parokia kwa kuwa hapakuwa na Parokia eneo hili kwa mahitaji pana ya Kanisa.
Padre Dominico aliporudi na ujumbe wa Baba Kadinali na kuwaeleza Viongozi wake wa Shirika ndipo taratibu za kuanza Ujenzi wa Kanisa la Mt. Gaspar Del Bufalo ulianza, Michoro ya Kanisa ilichorwa kutoka Italia na ndugu wa Padre Dominico Altieri na hapa kwetu ilitafsiriwa na Kusimamiwa na Mhandisi Joseph Chuwa kama (Structural Engineer) kwa Kujitolea na Mjenzi ndugu Bertino (DRC) kwa kulipwa, Ufadhili kutoka Italia ulitengeneza Paa la Kanisa kutoka Kiwandani pamoja na mabati yake.

Mwaka 2001 mwezi Julai Padre Dominico Altieri alihamishiwa Italia, Padre Denis Massawe alimpokea uongozi kama Paroko wa Parokia ya Mt. Nicholaus Kunduchi ambapo walikuwa wanahudumia pia Kigango cha Mt. Gaspar Del Bufalo, Padre Denis Massawe alisimamia Ujenzi wa Kanisa la Mt. Gaspar Del Bufalo baada ya kuweka msingi na Jamvi la Kanisa Padre Denis Massawe alihamishiwa Dodoma (Miyuji) na nafasi yake ilichukuliwa na Padre Alponce Minja ambaye aliendeleza Ujenzi kwa kusaidiana na Mhandisi na wanakigango cha Mt. Gaspar Del Bufalo Pamoja na wanaparokia wote wa Mt. Nicholaus Kunduchi.

Tarehe 11 Mwezi March Mwaka 2007 Kigango cha Mt. Gaspar Del Bufalo kilipewa hadhi ya kuwa PAROKIA na aliyekuwa ASKOFU MKUU WA JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM HAYATI MWADHAMA POLCARP KARDINALI PENGO chini ya Padre Gregory Mkhotya Paroko wa kwanza. Viongozi Kamati Tendaji Parokia waliokuwepo Parokia ilipotangazwa walikuwa:

MWENYEKITI- LAURENT KALUGIRA
MAKAMU M/KITI- THADDEI MLINGI
KATIBU - FLORIAN NGUNANGWA
K/MSAIDIZI- AGNESS SHENGENA

MTUNZA HAZINA- PETRONILA LAWI

Mwaka 2009 Padre Gregory Mkhotya alihamishwa na aliyekuwa Paroko Msaidizi Padre Patrick Kimaro alikabidhiwa Parokia. Padre Patrick aliendeleza kazi ya ujenzi wa kanisa ikiwemo kuweka **picha za watakatifu ndani ya kanisa** zilizotengenezwa India, kuweka nakshi Altare(**Mosaic) , kujenga Mnara wa Kengele na kujenga Uzio** baada ya kukamilisha ujenzi wa kanisa na kuweka mahitaji yote mhimu **KANISA LILITABARUKIWA TAREHE 24.10.2015 NA ASKOFU MKUU WA JIMBO KUU LA DAR ES SALAAM MWADHAMA POLCARP KARDINALI PENGO (ASKOFU MKUU MSTAAFU KWA SASA**) Katika kutimiza ndoto ya waliokuwa viongozi wa shirika la Wamisionari wa Damu Azizi ya Yesu kutoka Italia ya Kujenga **SHRINE,** Padre Patrick kimaro kwa kushirikianana Uongozi wa Kamati Tendaji Parokia na wanaparokia wote, Walianzisha ujenzi wa Makazi ya Hija ulioanza rasmi **mwaka 2018**.

Mwaka 2019 Padre Patrick Kimaro alihamishwa kwenda Jimbo Katoliki la Singida na nafasi yake ilichukuliwa na Padre Thaddeus Memba ambaye ni Paroko hadi sasa. Katika kuhakikisha Maono ya viongozi wa shirika, Padre Thaddeus Memba aliendeza ujenzi wa Makazi ya Hija ambayo kwa sasa yapo kwenye hatua ya kukamilisha (Finishing), Pia alikuja na Mpango Mkakati wa kuhakikisha kweli Kituo cha Hija kinakuwa na Vivutio vya kiroho ambavyo vitawafanya Waamini wafike hapa Parokiani kwa ajili ya Kuhiji Vivutio hivyo ni: **Ujenzi wa Vituo vya Njia ya Msalaba Nje ya Kanisa (Fiber), Kuchora Rosari ya Damu Azizi ya Yesu, Ujenzi wa Grotto la Mama Bikira Maria Ambalo linavutia ukienda kusali unamkuta, Bikira Maria Mama wa Damu Azizi, Bikira Maria Mpalizwa Mbinguni na Bikira Maria wa Fatima, kufanya Upanuzi wa nyumba ya Mapadre, Ujenzi wa Kanisa Dogo la Kuabudu Damu Azizi ya Yesu (Adoration Chapel**).

2: UONGOZI WA PAROKIA

1. PAROKO – PADRE THADDEUS MEMBA CPPS
2. WASAIDIZI- PADRE FLORENCE KISSIMA CPPS
   PADRE BENEDICT MAGABE CPPS
   PADRE DENNIS MASSAWE CPPS

VIONGOZI WA KAMATI TENDAJI PAROKIA WA SASA

MWENYEKITI SIMON NJAU
MAKAMU M/KITI ADELINE MOSHI
KATIBU PIUS NYANDA
K/MSAIDIZI THEA MUSHI
MTUNZA HAZINA RENATHA RUGARABAMU

MAWASILIANO YA PAROKIA.

0748455455
Email: *gasparparish@yahoo.com*

3: RATIBA ZA HUDUMA PAROKIANI
UTARATIBU WA MISA SIKU ZA WIKI NA JUMAPILI

JUMATATU - IJUMAA
SAA 12:00-12:30 ASUBUHI
SAA 1:00 – 1:30 ASUBUHI
SAA 11:00 JIONI

JUMAMOSI NA SIKUKUU
SAA 12:30 ASUBUHI

JUMAPILI
MISA YA KWANZA
SAA 11:30 – 1:00 ASUBUHI
MISA YA PILI
SAA 1:15 - 3:15 ASUBUHI
MISA YA TATU {ENGLISH MASS}
SAA 3:30 - 5:00 ASUBUHI {9:30- 11:00AM}
MISA YA NNE
SAA 5:30 -7:00 MCHANA
MISA YA TANO
SAA 11:00 JIONI

MAUNGAMO-KILA SIKU NA MUDA WOTE WA KUABUDU

KUABUDU- KILA SIKU SAA 1:00 -2:00 USIKU {ADORATION CHAPEL}

HUDUMA ZA KIOFISI
JUMANNE- **JUMAMOSI** SAA 2:30 ASUBUHI - 6:00 MCHANA
SAA 9: 00 ALASIRI – 11:30 JIONI

JUMATATU OFISI HAZIFUNGULIWI ISIPOKUWA KWA SHIDA YA DHARURA

NB: MATATARISHO YA NDOA MIEZI MITATU KABLA YA KUFUNGWA, NDOA HAZIFUNGWI IJUMAA WALA JUMAPILI.

Huduma nyingine zinazopatikana katika parokia yetu

1. Adoration chapel (kuabudu damu azizi ya yesu)
2. Vituo vya njia ya msalaba nje ya kanisa
3. Grotto kubwa ya mama bikira maria watatu (bikira maria mama wa damu azizi, bikira maria wa Fatima na bikira maria mpalizwa)
4. Jengo la makazi ya hija (hostel na kumbi) kwa ajili MAHUJAJI







KANISA LA MT. GASPAR DEL BUFALO







KANISA DOGO LA KUABUDU DAMU AZIZI (ADORATION CHAPEL)



GROTTO LA BIKIRA MARIA





MNARA



KITUO CHA NJIA YA MSALABA



JENGO LA MAKAZI YA HJI



NYUMBA YA MAPADRE



OFISI ZA PAROKIA



UKUMBI WA MAKUTI



KANTINI.